# NISHATI
HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin


www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

**Toleo Namba 34** — **Januari 1 - 31, 2022**



# JNHPP KUTEKELEZWA KWA WELEDI, UFANISI, WAKATI NA GHARAMA ZILIZOPANGWA – MAKAMBA








## HERI YA MWAKA MPYA 2022

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**



# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Leonard Masanja**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**

Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma








*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,
WIZARA YA NISHATI

# HERI YA MWAKA MPYA 2022

**UONGOZI WA WIZARA YA NISHATI PAMOJA NA WAFANYAKAZI, WANAWATAKIA WATANZANIA WOTE HERI NA FANAKA KATIKA MWAKA 2022.**

***"Nishati kwa Maendeleo ya Viwanda na Ukuaji wa Uchumi"***

# JNHPP KUTEKELEZWA KWA WELEDI, UFANISI, WAKATI NA GHARAMA ZILIZOPANGWA – MAKAMBA



*Waziri wa Nishati, January Makamba na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato pamoja na ujumbe kutoka Misri wakikagua Mdari wa Umeme wa Julius Nyerere.*

**Na Dorina G. Makaya – Rufiji, Pwani.**

Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba amesema Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere (JNHPP) unatekelezwa kwa weledi, ufanisi, wakati na gharama zilizopangwa

Waziri Makamba aliyasema hayo tarehe 07 Novemba 2021, akiwa kwenye ziara ya kikazi na Waziri wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri Mhe. Mhandisi Assem Hafez El Gazar walipotembelea Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) tarehe 07 Desemba, 2021.

Alieleza zaidi kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati inasimamia mradi huo mkubwa wa Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius (JNHPP) na kuwa mradi huo unagharamiwa kwa fedha za Watanzania shilingi trilioni 6.558 na utazalisha umeme wa Megawati 2,115.

Waziri Makamba pia alikumbushia kuwa, ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere (JNHPP), ni muhimu na ni mradi mkubwa wa kimkakati kwa nchi yetu. "Sisi kama wasimamizi tumepewa jukumu na Rais wetu Mhe Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kwa weledi, ufanisi, wakati na gharama zilizopangwa" alisema Waziri Makamba.

Alikumbushia kuwa, wakandarasi wa mradi huo wametoka katika nchi ya Misri na kuwa ziara hiyo ya Waziri wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri Mhe. Mhandisii Assem Hafez El Gazar, aliyepewa dhamana ya kusimamia Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius (JNHPP), inaonyesha namna ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ilivyochukulia kwa uzito wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba Mradi unatekelezwa kwa weledi, ufanisi, wakati na gharama zilizopangwa

"Tumekuja hapa leo kukagua maendeleo ya mradi, kuangalia tulipofikia, kuangalia kama kuna

# JNHPP KUTEKELEZWA KWA WELEDI, UFANISI, WAKATI NA GHARAMA ZILIZOPANGWA – MAKAMBA

changamoto kwa upande wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Misri ili tuweze kutatua na kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu." Alisema Waziri Makamba.

Waziri January Makamba alisema, baada ya kutembelea mradi, waliona unaendelea vizuri pamoja na changamoto chache zilizopo za Mradi kutokwenda kwa kasi kama iliyokuwa imepangwa. Lakini, alieleza kuwa si jambo la ajabu kutokea kwa miradi mikubwa kama huo kuchelewa kukamilika.

Alisema, jambo jema ni kuwa, mradi uko katika hatua nzuri ya utekelezaji na iwapo italazimu kuongeza muda basi utakuwa ni muda unaokubalika na hakutakuwa na gharama za ziada.

"Sisi tumepewa kazi ya kuhakikisha kwamba mradi unatekelezwa na kukamilika kwa kuzingatia usalama na ubora na kutuhakikishia upatikanaji wa umeme wa uhakika. alisisitiza Waziri Makamba.

Naye Waziri wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Mhe. Mhandisi Assem Hafez El Gazar alisema, Mradi wa JNHPP ni muhimu sana kwa nchi zote mbili za Tanzania na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri.



*Waziri wa Nishati, January Makamba na Waziri wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Misri, Mhandisi Assem Hafez El Gazar wakiwa katika eneo la mdari wa Umeme wa Julius Nyerere.*

Alibainisha kuwa, wakati alipoteuliwa kushika nafasi hiyo ya Uwaziri wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, maelekezo ya kwanza aliyopewa ni kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP)

Waziri El Gazar aliuelezea Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) kuwa ni mradi utakaosaidia kuimarisha mahusiano baina ya nchi hizo mbili na kuwa, ukitekelezwa vizuri utajenga imani kwa watanzania kuwa, Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ni nchi yenye uwezo wa kutekeleza miradi mingine mikubwa.

Aidha, Waziri huyo wa Nyumba, Huduma na Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri Mhe. Mhandisi Assem Hafez El Gazar, aliwataka wakandarasi wajitahidi kukamilisha mradi huo kwa wakati na ubora unaokubalika.

# HATUA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI MRADI WA UMEME WA MAJI WA JULIUS NYERERE








# NISHATI JADIDIFU KUPUNGUZA UHARIBIDU WA MAZINGIRA




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza katika Mkutano wa wadau wa Nishati jadidifu na uzinduzi wa miradi ya Nishati jadidifu,uliofanyika jijini Dodoma Desemba 13,2021.*

**Hafsa Omar- Dodoma**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema Serikali itahakikisha kuwa Nishati Jadidifu itakuwa moja ya chanzo kikubwa cha kuzalisha nishati nchini ili kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira nchini.

ALIyasema hayo, Desemba 13, 2021 wakati wa Mkutano wa wadau wa Nishati jadidifu na uzinduzi wa miradi ya Nishati jadidifu,uliofanyika jijini Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuzindua miradi hiyo ya nishati jadidifu, alisema kuwa nishati mbadala ni nishati ambayo inafaida kubwa ya kutochafua mazingira kwa upana wake na ina faida ya kutumika kidogo na kufanya kazi kubwa.

" tumezindua miradi miwili, mradi wa kwanza unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya lakini unapewa fedha na UN unalenga kuhakikisha kunakuwa na matumizi machache ya kuni na mkaa katika maeneo yetu, na mradi wa pili tuliozindua ni mradi unaolenga Zaidi kwenye kilimo lakini kwa kutumia umeme jua miradi yote hii imelenga katika matumizi sahihi ya nishati jadidifu", alisema.

Alifafanua kuwa, mradi huo uliojikita kwenye matumizi ya Nishati safi ya kupikia, utaanza kutekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza ambapo imeelezwa kuwa katika majiji hayo mkaa unatumika kwa kiwango cha juu kulinganisha na mikoa mengine, ambapo mkoa wa dar es salaam unaongoza kwa




*Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Manfredo Fanti, akizungumza katika Mkutano wa wadau wa Nishati jadidifu na uzinduzi wa miradi ya Nishati jadidifu,uliofanyika jijini Dodoma Desemba 13,2021.*

matumizi ya mkaa kwa asilimia 50 ya mkaa wote unaotumika nchini.

Sambamba na hilo, alisema Wizara imejipanga kuhakikisha kuwa mwaka huu inazalisha megawati 150 kutoka kwenye vyanzo vya nishati jadidifu kwa maana ya jua na upepo na tayari Serikali imeanza kusaini mikataba na wawekezaji mbalimbali ili kuanza kutekeleza miradi hiyo.

Pia, Serikali imejipanga ifikapo mwaka 2025 kwa kutumia vyanzo mbalimbali ambavyo vipo nchini kuzalisha megawati 1100 zitokanazo na nishati jadidifu jambo ambalo litawezekana kwasababu kunampiango mizuri iliyopo na utekelezaji wake unaonekana.

Kwa upande wake, Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Manfredo Fanti, alisema kuwa Mradi ambao umezinduliwa ni sehemu ya mashirikiano baina ya Umoja wa Ulaya na Tanzania kwa upande wa sekta ya nishati.

Aidha, alisema mradi huo ni muhimu kwasababu utatoa mchango mkubwa katika kupunguza matumizi ya mkaa hasa katika maeneo ya mjini na vijijini.

Vilevile, amefafanua kwamba mradi huo hautasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira tu lakini pia utasaidia kuimarisha afya za watu kwakuwa hewa itokanayo na moshi wa matumizi ya mkaa na kuni unamadhara kwa afya ya mtumiaji.

# NISHATI JADIDIFU KUPUNGUZA UHARIBIDU WA MAZINGIRA



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (tatu-kushoto) akikata utepe kuashiria kwa uzinduzi wa mradi wa Matumizi safi ya Nishati ya kupikia, uliofanyika jijini Dodoma Desemba 13,2021.*





*Picha za mtukio mbalimbali katika Mkutano wa wadau wa Nishati jadidifu na uzinduzi wa miradi ya Nishati jadidifu,uliofanyika jijini Dodoma Desemba 13, 2021.*

# WATAALAM WAKUTANA KUANDAA MKAKATI WA USIMAMIZI RASILIMALI MAJI

**Hafsa Omar-Morogoro**

Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo Desemba 17, mwaka huu, wamekutana mkoani Morogoro ili kuandaa mkakati wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu ya Umeme nchini.

Katika kikao hicho ambacho wataalam hao waliwasilisha mada mbalimbali ambazo zitasaidia kuwezesha kuwa na mkakati madhubuti wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde tajwa.

Akizungumza kwa Niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangira, alisema kutokana na umuhimu wa vyanzo vya maji kwa ajili ya mito inayotiririsha maji katika mabonde tajwa na kuzingatia wajibu wa Wizara ya Nishati katika ufanisi wa vituo na miradi ya Umeme.



*Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangira akizungumza katika kikao cha Waatalam kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo Mkoani Morogoro Desemba 17, 2021.*

Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kwa nyakati tofauti walitembelea maeneo ya vyanzo vya maji katika bonde la Rufiji na kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo hayo kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo vya maji na matumizi fanisi ya rasilimali maji.

Aidha, Mhandisi Rwebangira, aliyataja maeneo ambayo Wizara imeratibu utoaji wa elimu husika, ni Mkoa wa Mbeya, Njombe, Iringa, Morogoro, Tabora, Singida, Dodoma na Pwani.

" kutokana na umuhimu wa mabonde haya kwa Taifa, na kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa yaliyotolewa kwa nyakati tofauti, ni wakati muafaka wa waatalam kutoka sekta mbalimbali kutafakari kwa kina na kwa pamoja na kuishauri Serikali mkakati Madhubuti wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde hayo",alisema.

Alibainisha kuwa, Asilimia 36 ya nishati ya umeme unaozalishwa nchini megawati 573 inatokana na chanzo cha maji ambapo vituo vikubwa vya kuzalisha umeme huo pamoja na madakio ya maji yapo ndani ya mabonde ya Pangani na Rufiji.

Aliongeza kuwa, ili kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu, Serikali imeendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia chanzo cha maji kutokana na unafuu wa gharama za uzalishaji ikilinganishwa na vyanzo vingine

# WATAALAM WAKUTANA KUANDAA MKAKATI WA USIMAMIZI RASILIMALI MAJI

vilivyopo nchini.

Alisema, Wizara ya Nishati ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zinazowezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika na unaotabirika kwa gharama nafuu kwa lengo la kuwezesha ustawi wa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

Alifafanua kuwa, katika jitihada hizo za kuendeleza uzalishaji umeme wa maji, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere wa megawati 2,115 na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya Ruhudji megawati 358 na mradi wa Rumakali wa megawati 222 yanaendelea.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa Bwawa la kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere (JNHPP) kutoka Wizara ya Nishati, Christopher Bitesigirwe, awali akiwakaribsha wataalamu hao alisema, lengo la kikao hicho ni kukaa pamoja na wataalam hao ili kuweza kuja na mkakati ambao utakuwa wa usimamizi rasilimali maji ya mabonde wa Rufiji na Pangani.

Pia, aliwataka watalam hao kutoa michango yenye tija ambayo itakuwa na manufaa katika Taifa la Tanzania.







*Wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo wakiwa katika kikao cha kuandaa mkakati wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani mkoani Morogoro Desemba 17,2021*

# NAIBU WAZIRI NISHATI, WAKILI STEPHEN BYABATO AKAGUA MIUNDOMBINU YA KUPOKELEA MAFUTA JIJINI DAR ES SALAAM

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amefanya ziara ya kukagua miundombinu ya kupokelea mafuta iliyoko Kigamboni na Kurasini (KOJ) jijini Dar es Salaam. Lengo likiwa ni kuona utendaji kazi katika eneo hilo.

Wakili Byabato amefanya ziara hiyo Desemba 17, 2021 akiambatana na Uongozi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja( PBPA) na Maafisa kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).









*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (mwenye suti ya Bluu) akikagua miundombinu ya kupokelea mafuta Kurasini na Kigamboni,jijini Dar es Salaam kwa lengo na kuona utendaji kazi katika eneo hilo, Desemba 17, 2021.*

# NAIBU WAZIRI NISHATI, WAKILI STEPHEN BYABATO AKAGUA MIUNDOMBINU YA KUPOKELEA MAFUTA JIJINI DAR ES SALAAM





*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato( mwenye suti ya Bluu) akikagua mifumo ya Kompyuta inavyofanya kazi katika eneo la kupokelea mafuta Kurasini na Kigamboni jijini, Dar es salaam, wakati wa ziara yake ya kuona utendaji kazi katika eneo hilo, Desemba 17,2021.*







*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (mwenye suti ya Bluu) akipata maelezo katika meli iliyokuwa inapakua katika eneo la Kurasini( KOJ), jijini Dar es salaam, wakati wa ziara yake ya kuona utendaji kazi katika eneo hilo, Desemba 17,2021.*

# MATUKIO KATIKA PICHA ZIARA YA NAIBU WAZIRI WA NISHATI MBAGALA, DAR ES SALAAM

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amefanya ziara ya kukagua miundombinu ya kupokelea mafuta iliyoko Kigamboni na Kurasini (KOJ) Jijini Dar es Salaam. Lengo likiwa ni kuona utendaji kazi katika eneo hilo.

Wakili Byabato amefanya ziara hiyo Desemba 17, 2021 akiambatana na Uongozi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja( PBPA) na Maafisa kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(kulia) akitoa maelekezo kwa Uongozi wa Shirika la Umeme( TANESCO), Wilaya ya Mbagala pamoja na wasimamizi wa Kituo cha Kusambaza Umeme cha Mbagala, wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho Jijini Dar es salaam, Desemba 16, 2021.*





*Msimamizi wa Kituo cha Kusambaza Umeme cha Mbagala, Mhandisi Neema Ngogo( wa pili kulia) , akimuonyesha Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato( wa pili kushoto) namna ambavyo umeme unapokelewa, kupozwa na kusambazwa kituoni hapo, wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho Jijini Dar es salaam, Desemba 16, 2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akipata maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Kituo cha Kusambaza Umeme cha Mbagala, Mhandisi Neema Ngogo, wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho Jijini DSM Desemba 16, 2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) akizungumza na Uongozi wa Shirika la Umeme (TANESCO), Wilaya ya Mbagala pamoja na wasimamizi wa kituo cha kusambaza Umeme cha Mbagala, baada ya kumaliza ziara ya kutembelea Kituo hicho, Jijini Dar es salaam, Desemba 16, 2021.*

# KIKAO CHA WATAALAMU CHAHITIMISHWA RASMI MJINI MOROGORO



*Mhandisi Yusuph Msembele kutoka Wizara ya Nishati(kushoto) Dkt. Richard Muyungi kutoka Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO) wakiwa kikao cha wataalamu, kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo kimehitimishwa rasmi mjini Morogoro.*

**Hafsa Omar-Morogoro**

Kikao cha wataalamu, kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo kimehitimishwa rasmi mjini Morogoro.

Kikao hicho, cha kuandaa mkakati wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu ya Umeme nchini, kilihitimishwa na Mratibu wa Mradi wa Bwawa la kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere (JNHPP) kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher Bitesigirwe.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhandisi Bitesigirwe aliwapongza wataalam hao kwa ushirikiano wao walionesha katika kipindi chote cha kufanya kazi hiyo.

Aidha, aliwataka kuendelea na ari hiyo ya ufanyaji kazi katika kipindi chote cha uaandaji na utekelezaji wa kazi hiyo mpaka pale itakapokamilika.

Pia, aliwasisitiza kutekeleza mambo yote ambayo kikao hicho kimeadhimia ili kuweza kufanikisha kazi hiyo ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa kiujumla.



*Mratibu wa Mradi wa Bwawa la kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere (JNHPP) kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher Bitesigirwe akizungumza wakati wa kuhitimisha kikao cha wataalam, kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo kimehitimishwa rasmi mjini Morogoro.*

Vilevile, aliwashukuru kwa kujitoa na kuhakikisha kuwa kazi hiyo inafanyika kwa mafanikio makubwa ambayo yatasaidia katika utekelezaji wake.

"Nichukue fursa hii kuwashukuru sana, kwa michango na mawazo yenu, michango yenu hii ni muhimu sana hasa katika kuandaa huu mkakati wa usimamizi wa rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani, michango hii itasaidia kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu ya Umeme hapa nchini"alisema.

Kwa upande wake, Martha Ngalowera kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, alisema kuwa mpango huo utakapo kamilika na kuanza utekelezaji wake utakuwa ni msaada mkubwa kwaajili ya kuzalisha umeme endelevu nchini.



*Wakati wa kuhitimisha rasmi kikao cha wataalam, kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo kimefungwa rasmi mjini Morogoro.*





*Picha za Matukio mbalimbali wakati wa kuhitimisha rasmi kikao cha wataalamu, kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo kimefungwa rasmi mjini Morogoro.*

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*